Wapelelezi 12

TRUEWAY KIDS.COM

Utangulizi

Video playlist

Juma hili tutaendelea kufuatilia simulizi/habari ya Waisraeli baada ya kutoka Misri. Somo letu litagusia kuhusu wapelelezi 12 waliokwenda kupeleleza Nchi ya Ahadi. Somo letu litapatikana katika kitabu cha Hesabu 1-3 na Hesabu 13-14. Baadhi ya pointi za kuzingatia ni:

- Yoshua na Kalebu waliona watu wa kuwatisha lakini walichagua kumwamini Mungu. Pia tunaweza kumuamini Mungu nyakati za kutisha
- Mungu ni mkubwa na mwenye nguvu sana kuliko kitu kingine chochote au mtu yeyote.
- Tunapaswa kuweka macho yetu kwa Mungu kuliko vitu vinavyo tutisha/ tuogopesha.
- Watu walichagua kuwaamini wapelelezi 10 badala ya kumwamini na kumtegemea Mungu. Tunapaswa kumwamini Mungu kwa sababu siku zote hutunza ahadi Zake.

Muongozo wa Somo

Wakumbushe watoto wako kwamba Waisraeli walikuwa wakielekea katika nchi mpya na Mungu alikuwa wakiwaongoza kwa nguzo ya moto na ya wingu.

Waulize watoto kama waliwahi kuogopa. Zungumzieni kuhusu vitu wanavyoviogopa. Waeleze kila mtu ana kitu anachokiogopa, lakini Mungu anaweza kutupatia ujasiri/ushujaa.

Jaza hewa puto/pulizo. Tumia kalamu ya rangi kuchora baadhi ya vitu mnavyoviogopa. (Zinaweza kuwa picha rahisi). Waeleze ni namna gani vitu hivyo vinavyo tisha vinaonekana vikubwa. Chukua kitu chenye ncha kali na utoboe pulizo kutoa hewa nje. Waonyeshe namna hofu “nyingi” si kitu, ni kama hewa tu. Tumia mfano huo kumuonyesha mtoto namna huwa tunaogopa kitu wakati hatukupaswa kuogopa; ya kwamba tunapokuwa na Mungu, hatupaswi kuogopa.

Mungu alitaka kuwapanga/kuwaandaa watu wa Israeli na kuwahesabu. Waelezee watoto kwamba kupanga inamaana kuweka vitu katika mpangilio mzuri na sensa ina maana kupata hesabu ya watu. Itategemea na umri wa mtoto wako, mnaweza kufanya hesabu ya wanasesere wake na kuwapanga.

Kusanya vitu kumi na mbili (sarafu, kokoto, marumaru na kadhalika.) vitu vyenye uzito sawa na kimoja kizito zaidi. Tengeneza mizani rahisi-weka henga kwenye kitasa cha mlango. Kila upande, funga kamba pamoja kisha kila mwisho wa kamba funga kikombe. Katika somo, hili unaweza kutumia mizani hiyo kupimia vitu hivyo, (maelezo zaidi yanapatikana mtandaoni).

Hesabu wakati unaweka vitu viwili katika upande mmoja na kumi katika upande mwingine. Waonyeshe namna vitu kumi vinazidi uzito vitu vile viwili. Chukua kitu kizito zaidi na uweke ndani ya kibombe pamoja na vitu viwili. Mizani italemea upande huo. Tumia mfano huo kuonyesha chaguzi za Mungu zinapaswa kubeba uzito zaidi ya chaguzi zetu. Mkumbushe mtoto kwamba haijalishi watu wengine watasema nini, kile Mungu amesema kitabaki kuwa sahihi.

Sali na mtoto na umuombe Yesu akusaidie uweze kusimama thabiti bila uoga kwa kile Mungu amesema.

© 2022 truewaykids.com



Watu wakaanza kulalamika na kulia, “Mungu hawezi kutusaidia.”

Musa aliwakumbusha watu kwamba Mungu ni mkubwa na mwenye nguvu kuliko kitu chochote.

Lakini watu hawakusikiliza.

Mungu akasema, watu watazunguka nyikani kwa miaka arobaini.

Ni Kalebu na Yoshua pekee ndio watakaoingia Nchi ya Ahadi.

Wapelelezi 12

Siku moja Mungu alimwambia Musa, “ni muda wa kutuma baadhi ya wanaume wakapeleleze nchi ya Kanaani.”

Mungu aliahidi kwamba atawaongoza Waisraeli hadi nchi ya ahadi yenye asali na maziwa. Kiongozi mmoja kutoka katika kila kabila alichaguliwa kwenda kupeleleza nchi.



Wapelelezi kumi na mbili waliondoka na kwenda katika Nchi ya Ahadi.

Walisafiri kwa siku arobaini wakiiangalia nchi ambayo waliahidiwa.

Walikata baadhi ya mizabibu kutoka katika miti ya mizabibu. Vishada/ vichane vya mizabibu vilikuwa vikubwa sana, wanaume wawili walipaswa kubeba!

Wapelelezi walirudi. "Ni nchi nzuri sana," walisema.



Lakini waliendelea, "lakini watu wa mji ule ni wakubwa sana na miji yao ni thabiti na imezungushiwa maboma/ ukuta. Hatutaweza kuwashinda.
Kalebu, mmoja wa wapelelezi alisema, "Mungu akiwa upande wetu, tutawashinda majitu." Yoshua, mpelelezi mwingine alisema, "Nakubaliana na Kalebu."
Lakini wengine walikuwa wanaogopa sana.
Waliondoka na kwenda kuwaambia watu, "Majitu yana nguvu sana."

Kazi na Michezo

Mchezo wa mpelelezi-1

Wasaidie kuwaelewesha nini maana ya mpelelezi kwa kucheza na mtoto wako, “nakupeleleza.”

Inategemea na umri, mnaweza kutumia herufi au rangi.

Karamu ya matunda

Nchi ya Ahadi ilikuwa na maziwa, asali na matunda matamu.

Kwa nini msipate viburudisho na matunda anayopendelea mtoto wako.

Mshukuruni Mungu kwa pamoja kwa kuwapa vitu vya kufurahia.

Kuhesabu wanasesere

Ni bahati nzuri kama mtoto wako atafahamu sensa ni nini, lakini watafahamu kuhesabu na kupanga ni nini.

Tumia wanasesere au vitu vya kuunda/vya ufundi. Pangeni vitu kwa pamoja. Kwa mfano: wanasesere wa magari, rangi na vitu vinginevyo.

Halafu hesabuni kila kimoja kujua idadi yake.

© 2022 truewaykids.com

Jigsaw ya Nchi ya Ahadi

Kata picha zilizo katika karatasi ili kutengeneza jigsaw.

Ziweke pamoja ili kukumbuka kile wapelelezi walikipata katika Nchi ya Ahadi.







© 2022 truewaykids.com

Kubwa au ndogo

Paka rangi kifaa kikubwa kwa rangi ya bluu.

Paka rangi kifaa kidogo kwa rangi nyekundu.













© 2022 truewaykids.com

Chora na kupaka rangi, nyuso 10 zenye huzuni na 2 zenye furaha.

12

© 2022 truewaykids.com

Tafuta vitu hivi vifuatavyo katika picha.

© 2022 truewaykids.com

Zabibu za asili

Juma hili nataka tufanye kazi ya mikono/ufundi utakaochanganya wapelelezi watakao kwenda ndani ya nchi ya ahadi ili kuona watapata nini kwa kutumia ufundi halisi. Sehemu ya kwanza ya kazi ya mikono itahusisha matembezi ya kawaida kutafuta vitu/vipengele vifuatavyo.

Utahitaji nini:

- boksi nene
- gundi ya maji
- kitawi (kitawi chenye vijitawi vidogo vidogo), majani, mawe madogo, (tumia fikira zako)
- rangi ya kupaka ya zambarau

Nini kifanyike:

Fanyeni matembezi vichakani au bustanini ili kupata vitu vilivyo katika picha.

Weka vitu vyako vyote pamoja na panga namna ya picha.

Paka gundi juu ya boksi lako na uanze kugundisha vitu.

Paka gundi katika umbo la pembe tatu na unyunyize mchanga/ changarawe kufanya mizabibu.

Ongeza majani na vitu vingine vya asili.

Itakapokauka, unaweza kuongeza maelezo kwa rangi. Kwa mfano, kupaka rangi zabibu.

© 2022 truewaykids.com

© 2022 truewaykids.com



© 2022 truewaykids.com

© 2022 truewaykids.com



© 2022 truewaykids.com



Muda wa kuabudu

Agiza kuimba wimbo wa kuabudu. Siyo ulioandaliwa na Trueway Kids.
Video za Yutube zitumike kwa matumizi binafsi tu.

My God is so big

https://youtu.be/Bha0hAUqJ_U

Be bold, Be strong

https://youtu.be/zRvCUz6KFB4

Strong and Courageous

https://youtu.be/t34ajxa7TCI

Muda wa maombi

Mshukuru Mungu kwamba ni Mwenye Uweza/nguvu, na kwake hakuna kinachoshindikana.

Muombe Mungu akusaidie uwe jasiri na umwamini Yeye.

Juma lijalo

Kuzunguka Nyikani

Kama bado hujafanya hayo, jiunge kwa barua pepe ili kupokea somo la wakati ujao.
truewaykids.com/subscribe/

© 2022 truewaykids.com